



**Office of the Chief Executive**

31 Flinders Street  
Adelaide SA 5000

GPO Box 1152  
Adelaide SA 5001  
DX 541

[www.education.sa.gov.au](http://www.education.sa.gov.au)

Wapendwa Wazazi na  
Welezi,

COVID-19 imeweka changamoto za kila aina kwa ajili yetu, kama watu binafsi, familia na jamii.

Tunajivunia kusema kuwa walimu wetu na wafanyakazi wa msaada wamechomoza katika tukio hilo. Licha ya wasiwasi wanazoweza kuwa wazipata kama washiriki wa jamii, wameweka mafunzo ya wanafunzi wao katika mstari wa mbele.

Shule na chekechea ni huduma mhimu. Ushauri wa afya ya umma kutoka kwa wataalamu wa ngazi za juu wa Australia hubakia kwamba wanaweza na wanapaswa kubaki mashuleni.

Tutaendelea kuongozwa na ushauri wa afya, na mapendekezo yao juu ya kujitenga kijamii na mazoea ya usafi katika madarasa yetu na nafasi za kucheza. Usalama na ustawi wa wanafunzi wetu, wafanyakazi na jamii ya shule ni kipaumbele cha juu kadri tunavyoendelea kutoa elimu ya ubora wa juu.

Wakati wengi wakiendelea kukaa nyumbani ili kusaidia kuzuia kuenea kwa COVID-19, sisi hatutasimama wima.

Kuendelea na mafunzo kwa watoto wetu na vijana katika hali hii linabakia kuwa lengo letu kuu. Walimu, waelimishaji wa shule za awali, wakuu wa shule na wafanyakazi wa Idara daima – kwa kuongeza matoleo yetu ya kusaidia familia na watoto katika nyakati hizi za changamoto.

Wiki iliyopita, tulianzisha Masomo Yetu ya SA (Our Learning SA) tovuti inayohifadhi mamia ya nyenzo za kufundishia kusaidia watoto na vijana kuendelea na mafunzo yao wakati wakiwa nyumbani. Pamoja ni viungo vya mipango ya ABC TV ambayo ni ya ubora wa juu na inaweza pia kusaidia mafunzo ya mwanafunzi. Itakuwa inaendelea kukua, hivyo tafadhali endelea kuangalia kwenye [www.ourlearning.sa.edu.au](http://www.ourlearning.sa.edu.au).

Pia tumeunda ushauri kwenye sehemu ya familia kwenye tovuti, ambayo ina video na karatasi za ukweli kwa wanafunzi na familia, ikiwa ni pamoja na:

- Kuweka mazingira ya kujifunza
- Kukaa na furaha na afya wakati wa kujifunza nyumbani
- Kusoma nyumbani na mtoto wako
- Kujitayarisha kwa mafunzo ya mtandaoni
- Kuzungumza na mtoto wako kuhusu COVID-19

Shule na vituo viko katika hatua tofauti katika utekelezaji wa mipango ya kujifunza kwa mbali. Kwa kuongezea, tunajua kuwa so kila mtoto ana kompyuta nyumbani, au kwenye mtandao.

Wiki hii, wakati wa siku nne za wanafunzi za kutokusoma, walimu wetu wanachukua mafunzo ya nyumbani kwenye ngazi inayofuata.

Tunafanya madarasa halisi yanayopatikana kwa kila mwalimu, na kuchunguza njia za kuwapata watoto wasio na kompyuta au intaneti iliyounganishwa na darasa lao. Hii inakwenda mkono kwa mkono na rasilimali za kufundishia za walimu ambao wamekuwa na bidii kujiandaa kwa ajili ya wanafunzi ambao wanaowahitaji.

Tunaendelea daima kuvutiwa na jinsi wafanyakazi wetu na waalimu wanashirikiana kujiandaa kwa ajili ya muhura wa 2. Sisi sote tuko katika hili pamoja.

Tafadhali fanya kazi na mwalimu wa mtoto wako kama unahitaji usaidizi wa ziada au una maswali yoyote.

Wako mpendwa,



Hon John Gardner MP  
**Waziri wa Elimu**

7 April 2020



Rick Persse  
**Mkurungezi Mkuu**

7 April 2020